TANGAZO LA SERIKALI NA. 785 la tarehe 3/11/2023

SHERIA YA HAKIMILIKI NA HAKISHIRIKI,
(SURA YA 218)

## KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 48A)*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA ADA YA HAKIMILIKI KWA VIBEBEO VYA KAZI ZA UBUNIFU VILIVYO TUPU ZA MWAKA 2023

Jina
T.S. Na. 385 la 2023

**1.** Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Ada ya Hakimiliki kwa Vibebeo vya Kazi za Ubunifu Vilivyo Tupu za mwaka 2023 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Ada ya Hakimiliki kwa Vibebeo vya Kazi za Ubunifu Vilivyo Tupu za Mwaka 2023 ambazo zitarejewa humu kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 1

**2**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 1 kwa kufuta maneno "Ada ya Hakimiliki kwa Vibebeo vya Kazi za Ubunifu Vilivyo Tupu" na kuweka maneno "Tozo ya Hakimiliki".

Marekebisho ya jumla

**3**. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kuondoa neno "ada" na kuweka neno "tozo" popote linapoonekana kwenye Kanuni.

Marekebisho ya kanuni ya 2

**4**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 2 kwa-

(a) kwa kuongeza tafsiri ya msamiati ufuatao kwa kuzingatia mtiririko wa kialfabeti:

Sura ya 399

"Mamlaka ya Mapato Tanzania" maana yake Mamlaka ya Mapato Tanzania iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania;"

(b) kufuta tafsiri ya msamiati "kibebeo kilicho tupu"; na

(c) kufuta maneno "kwenye vibebeo vilivyo tupu" yaliyopo katika tafsiri ya msamiati "ada ya hakimiliki" au "ada".

Marekebisho ya

**5**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa-

*Tangazo Na 7895 (Linaendelea)*

kanuni ya 3

(a) kufuta maneno "vilivyo tupu" yaliyopo katika maneno ya utangulizi;
(b) kufuta aya (d);
(c) kuongeza aya zifuatazo mara baada ya aya (c):

"(d) kifaa cha kunakili data katika CD;
(e) kifaa cha kunakili data kidijitali kupitia DVD;
(f) Vinyl;
(g) Mini Diski;
(h) Kumbukumbu ya SD;"; na

(d) kubadili mpangilio wa aya (e) na (f) kuwa aya (i) na (j), mtawalia.

Kuongezwa kwa kanuni ya 3A

**6.** Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya kanuni ya 3 kanuni ya 3A kama ifuatavyo:

"Thamani ya tozo ya hakimiliki Sura ya 147

**3A**. Thamani ya tozo ya hakimiliki inayotolewa chini ya kifungu cha 48A cha Sheria itaamuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 141 cha Sheria ya Usimamizi na Ushuru wa Bidhaa.".

Kufutwa na kuandikwa upya kwa kanuni ya 4

**7**. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya kanuni ya 4 kama ifuatavyo:

"Malipo ya tozo

**4**. Tozo inayopaswa kulipwa chini ya Kanuni hizi itatozwa kwa bidhaa zilizoingizwa nchini au zilizotengenezwa ndani ya nchi na waingizaji wa bidhaa au watengenezaji, kadiri itakavyokuwa.".

Marekebisho ya kanuni ya 5

**8**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 5, kwa-

(a) kufuta kanuni ndogo za (2) na (3); na
(b) kubadili mpangilio wa kanuni ndogo ya (1) kuwa kanuni ya 5.

Kufutwa kwa kanuni ya 8

**9.** Kanuni kuu zinarekebishwa-

(a) kwa kufuta kanuni ya 8;
(b) kubadili mpangilio wa kanuni ya 9 kuwa kanuni ya 8.

*Tangazo Na 7895 (Linaendelea)*

Dodoma,
1 Septemba, 2023

**DAMAS DANIEL NDUMBARO**
*Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo*